

MKATABA WA UPANGISHAJI ENEO LA BIASHARA NA OFISI:

Mkataba huu umetiwa saina leo²⁸.....Mwezi.....^{07/2022}.....

kati ya

Ndugu **JAMAL HUSSEIN ALLY** wa S.L.P. 72141, Dar es Salaam, ambaye ni "**Mpangishaji**" kwa upande mmoja.

na

LOW TIDE CONSTRUCTIONS COMPANY LTD wa S.L.P.72141, Dar es Salaam, ambaye ni "**Mpangaji**" kwa upande mwingine.

Mpangishaji kwa hiari yake na bila ya kulazimishwa au kushawishiwa amekubali kumpangisha mpangaji kwa hiari yake amekubali kupanga eneo lilopo katika Mtaa kiombo, Kata ya Kitunda wilaya ya Ilala, Dar es Salaam.


Katika Mkataba huu pande zote mbili zinakubaliana kama ifuatavyo:-

1. Mpangaji atalipa kodi ya pango ya Shilingi 400,000/= kwa mwezi. Kodi ya pango italipwa kwa mkupuo wa miezi 6 wakati wa kusaini Mkataba huu.
2. Mpangaji kwa kulipa kodi ya pango iliyobainishwa katika Kifungu cha 1 na kufuata masharti ya Mkataba Mpangaji anamhakikishia Mpangishaji kuwa ataishi kwa amani na utulivu.
3. Mkataba huu utakuwa wa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia tarehe 01 mwezi wa nane (08) , Mwaka 2022 hadi tarehe 01 Mwezi wa nane(08), 2023
4. Mpangaji atalipa gharama za umeme, maji pamoja na huduma nyingine za usafi wa mazingira.
5. Mpangaji atafanya usafi pamoja na kutunza mazingira ya chumba bila kufanya uharibifu wowote.
6. Mpangaji haruhusiwi kufanya matengenezo makubwa au kujenga chochote ndani au nje ya nyumba bila ridhaa ya Mpangishaji.
7. Mpangaji haruhusiwi kupangisha mtu mwingine. Jukumu hilo ni la Mpangishaji pekee kufanya hivyo ni kinyume na mkataba huu.

8. Mkataba huu utadumu kwa muda uliopangwa, mpangaji akivunja mkataba kabla ya wakati hatorudishiwa fedha yoyote na Mpangishaji akivunja anapaswa kumlipa salio mpangaji wake.
9. Mpangaji anapotaka kuhama atoe taarifa mwezi mmoja kabla na ahakikishe hana deni lolote la kodi, umeme, maji na huduma nyingine zozote la sivyo vitu vyake vitazuiwa kufidia gharama hizo.
10. Mkataba huu ukiisha na iwapo Mpangishaji atahitaji chumba yake mpangaji atajulishwa kwa notisi ya mwezi mmoja kabla.
11. Mpangaji atie saina baada ya kusoma, kuelewa na kukubaliana na masharti ya upangaji.

Mkataba huu umeshuhudiwa na kutiwa saina leo tarehe

MPANGISHAJI

SAHIHI: 

JINA: JAMAL HUSSEIN ALLY

SAHIHI: 

SIFA: MPANGISHAJI

TAREHE: 28 / 07 / 2022

MPANGAJI:

SAHIHI: 

JINA: LOW TIDE CONSTRUCTIONS COMPANY LTD.


SAHIHI: 

SIFA: MPANGAJI/MWENYE BIASHARA

TAREHE: 28 / 07 / 2022

MBELE YA

JINA: AHMED KARARA

SAHIHI: 

SIFA: MPANGAJI BIASHARA

TAREHE: 28 / 07 / 2022